



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



TAARIFA KWA UMMA

RAIS SAMIA AIPA MANISPAA BILIONI MBILI

Katika Mwezi Septemba 2022, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imeipatia Manispaa ya Lindi fedha jumla ya **TZS 1,990,000,000** kwa ajili ya mapinduzi makubwa ya uboreshaji wa elimu ya msingi na sekondari.

Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa **Mabweni, Mabwalo, Nyumba za Walimu pamoja na Madarasa**. Aidha kwa mara ya kwanza katika historia ya Manispaa, Mheshimiwa Rais ameleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa **shule za msingi mpya tatu (3)** ili kuondoa shule zilizochakaa.

Hali kadhalika, atika maandalizi ya kuhakikisha wanafunzi wote wa kidato cha kwanza mwaka 2023 Mheshimiwa Rais Samia ameleta fedha kwa ajili ya **ujenzi wa madarasa mapya 20** ili kila mtoto atakayechaguliwa kuingia kidato cha kwanza aingie darasani.

Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametimiza wajibu wake, ameonesha upendo wake kwetu. Tunawasihi wananchi wa Manispaa ya Lindi kutimiza wajibu wetu na kushiriki katika ujenzi wa miradi hii.

Miradi Iliyopata fedha ni pamoja na:

- 1. 250m Ujenzi Shule Mpya, Shule ya Msingi Kingurungundwa**
- 2. 250m Ujenzi wa Shule Mpya, Shule ya Msingi Rutamba ya Sasa**
- 3. 250m Ujenzi wa Shule Mpya, Shule ya Msingi Ruchemi**
- 4. 350m Ujenzi wa Mabweni 2, Bwalo na Nyumba Mipingo Sekond**
- 5. 40m Ujenzi wa Madarasa 2 Shule ya Msingi Mtumbikile**
- 6. 350m Ujenzi wa Mabweni 2, Bwalo, Nyumba Nangaru Sekondari**
- 7. 80m Ujenzi wa Madarasa 4 Shule Shikizi Maloo**
- 8. 400m Ujenzi wa Madarasa 20 ya Kidato cha Kwanza 2023**

imetolewa leo 30.9.2022 na:

Mkurugenzi wa Manispaa,
MANISPAA YA LINDI.